

Kwanini kabila la Dani na Efraimu hayaonekani yakiorodheshwa miongoni mwa yale makabila 12 ya Israeli katika Ufunuo 7?

SWALI: Yakobo aliyetwa ISRAELI:Alikuwa na wana 12 (Benyamini,Yusufu,Yuda,Lawi,Asheri,Isakari,Gadi,DANI,Zabuloni,Naftali ,Reubeni,&Simeoni) Ambao kabila za Taifa la Israeli ziliitwa kwa majina ya hao wana 12 wa Israeli. Wana wawili wa Yusufu, Benyamini na Manase nao pia wanatajwa kuwa miongoni mwa makabila ya ISRAEL..Hivyo wana wa watoto wakiume wa Yakobo (WALIOFICHWA KUTAJWA KAMA KABILA ZA ISRAEL.Mfano wa Manase & Efraimu) nao pia wakitajwa kama kabila za Israel, hilo ni ono tosha kwamba Nchi ya ISRAELI imeundwa na zaidi ya KABILA 12 hivi? (SWALI:Bwana Mungu anapoenda kuupachika mzeituni halisi kwenye shina lake kulingana na Warumi 11} tunafunuliwa watakaopata hii neema ya mzeituni halisi kupachikwa ni KABILA12 tu za ISRAELI tunazizoma kwenye Ufunuo7:

Swali hapo ni kwanini hapo KABILA LA DANIL na lile la Efraimu Yamenyimwa hiyo Neema (hayajatajwa hapo) kwenye hiyo ufunuo mlango wa 7?

JIBU: Shalom ndugu.. Makabila ya Israeli ni 12 tu, Efraimu na Manase, walihesabiwa tu miongoni mwa makabila 12 kwa upendeleo wa Yusufu kutoka kwa baba yake lakini makabila halisi yaani watoto wa Yakobo ni 12 tu, ambao wanatambulika kuliunda taifa la Israeli...na ndio wale

Kwanini kabila la Dani na Efraimu hayaonekani yakiorodheshwa
miongoni mwa yale makabila 12 ya Israeli katika Ufunuo 7?

ambao majina yao yanaonekana katika milango ya kuta za mji ule
Yerusalemu mpya..**(Ufunuo 21:12)**..

Hao ni wale watoto halisi 12 wa Yakobo, kama tu vile misingi ya mji ule
ilivyokuwa 12 kufunua wale mitume 12 wa Bwana... Sasa ni kwanini
Efraimu na Dani, hawaonekani pale kwenye **Ufunuo 7**...Sasa kitu cha
kutazama hapo ni kwamba kiuhalisi ni kabila moja tu halipo pale, nalo ni
kabila la DANI, lakini kabila la Efraimu lipo, ndio lile kabila la Yusufu
lililotajwa pale...Ikumbukwe kuwa Yusufu aligawanyika mara 2, Manase
na Efraimu, Haiwezekani liwepo kabila la Yusufu halafu tena liwepo
kabila la manase na Efraimu kwa mpigo, hapo basi Yusufu angepaswa
awe na watoto wengine tofuati na hao wawili ili atengeneze kabila lake
mwenyewe, lakini kama wale ni watoto wake, basi Kabila lake lazima
ligawanyike tu,..

Hivyo unapona Biblia inasema Kabila la manase halafu tena inasema
kabila Yusufu ujue basi alimaanisha kabila la manase na kabila la
Efraimu, vile vile unapona mahali biblia inasema Kabila la Yusufu
halafu tena kabila la Efraimu, basi ujue linamaanisha kabila la Manase
na kabila la Efraimu...

Soma **(Hesabu 1:32, 13:11)** Lakini tukirudi kwenye kabila la Dani
ambalo tunaona limeondolewa, biblia haijatao sababu ya moja kwa moja

Kwanini kabila la Dani na Efraimu hayaonekani yakiorodheshwa
miongoni mwa yale makabila 12 ya Israeli katika Ufunuo 7?

kwanini limetolewa, lakini tukirudi nyuma, tunaweza tukahisi sababu moja, kumbuka Mungu huwa hapendezwi na mambo maovu hususani uabuduji sanamu,..Na ukirudi kwenye agano la kale utaona ni kabila moja tu la Dani ndio lililokuwa ovu kiasi cha kutokumwogopa Mungu hadi kwenda kunyanyua sanamu na kuiweka katika mji wao (**soma *Waamuzi 18***)..Hilo likawa chukizo kufikia hatua ya Mungu kuwaondoa katika neema ya wokovu aliokusudia kuuleta baadaye juu ya Israeli,..Hiyo inaweza kuwa ni sababu mojawapo zinaweza kuwepo sababu nyingine tusizozijua, pengine hadi hapo Mungu atakapotufunulia..

Lakini katika ulimwengu ujao Dani atakuwepo, Efraimu na Manase watarudi chini ya viuno vya Baba yao Yusufu na kuhesabiwa kuwa kabila moja.

Ubarikiwe sana.

Mada Nyinginezo:

Kwanini kabila la Dani na Efraimu hayaonekani yakiorodheshwa
miongoni mwa yale makabila 12 ya Israeli katika Ufunuo 7?

UFUNUO: MLANGO WA 7 & 11

UFUNUO: MLANGO WA 14

MPAKA UTIMILIFU WA MATAIFA UTAKAPOWASILI.

CHAKULA CHA ROHONI.

SWALI LA KUJIULIZA!

USILITAJE BURE JINA LA BWANA!

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp

[Print this post](#)